JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA
MTIHANI WA KUHITIMU KIDATO CHA NNE

015 **ELIMU YA DINI YA KIISLAMU**

(Kwa Watahiniwa Walioko na Wasiokuwa Shuleni)

Muda : Saa 3 **Mwaka: 2021**

Maelekezo

1. Mtihani huu una sehemu A, B na C zenye jumla ya maswali **kumi na tatu (13).**
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu A na B na maswali **matatu (3)** kutoka sehemu C.
3. Sehemu A ina alama **ishirini (20)**, sehemu B alama **thelathini na tano (35)** na sehemu C ina alama **arobaini na tano (45).**
4. Simu za mkononi na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

2 101015 100018

csee2021

Scanned with CamScanner

SEHEMU A (Alama 20)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Katika kipengele (i) – (xv), chagua jibu sahihi kisha andika herufi yake katika kijitabu chako cha kujibia.

(i) Mtu aliyeelimika anatofautiana vipi na yule ambaye hajaelimika?
A Hatua za kielimu alizofikia.
B Wingi wa tafiti alizozifanya.
C Idadi ya miaka aliyotumia vyuoni.
D Ufanisi katika utendaji wake.
E Uwezo wa kujenga hoja na kuchambua.

(ii) Mtu aliye na imani kwa mujibu wa Uislamu anakuwa na sifa gani?
A Kukubaliana na mawazo ya jambo linalosadikika.
B Kuwa na uwezo wa kuvumilia maumivu ya maisha.
C Kujizuia na tamaa ya mambo ya anasa na starehe.
D Kuwa mpole na mnyenyekevu akitembea ardhini.
E Kujua au kuwa na hoja thabiti juu ya anachokiamini.

(iii) Ni kwa namna gani wanadamu wanahisi uwepo wa Mola muumba katika maisha yao?
A Kwa kuwa na akili tofauti na wanyama.
B Kwa kukutana na changamoto mbalimbali.
C Kwa kukosa kupata majibu kuhusu asili yao.
D Uwepo wa athari ya fitrah katika maumbile yao.
E Kwa kuibuka watu waliotoa habari za Mungu.

(iv) Kwa mujibu wa Uislamu, kwanini haiwezekani mtu kuishi bila ya kuwa na Dini?
A Sote ni viumbe wa Mwenyezi-Mungu (s.w).
B Dini ni utaratibu wa maisha ya wanadamu.
C Watu wote wanazaliwa na Dini za kimila.
D Dini ilifundishwa na Malaika wa Mungu.
E Dini ni imani ya Mungu muumba aliye juu.

(v) Zifuatazo ni maana za Dini katika Uislamu **isipokuwa**:
A Uwezo, mamlaka au utawala
B Itikadi au mfumo wa maisha
C Imani ya kuwepo Mola muumba
D Mila inayofuatwa na jamii ya watu
E Mfumo wa maisha ya akhera

Scanned with CamScanner

(vi) Fani ya Fiq'h inahusu mambo gani katika Dini ya Uislamu?

A Maarifa ya hukumu na sheria
B Historia ya dini ya Uislamu
C Itikadi ya upweke wa Allah (s.w)
D Imani juu ya mambo yasiyoonekana
E Hadithi na Sunnah za Mtume (s.a.w)

(vii) Njia ipi inakamilisha kupatikana kwa Ijtihaad kama msingi wa sheria za Uislamu?

A Qiyas + Ijmaa + Tafsiri ya wanazuoni
B Qur'an + Sunnah + Tafsiri ya wanazuoni
C Sunnah + Tafsiri ya wanazuoni + Qiyas
D Tafsiri ya wanazuoni + Qur'an + Qiyas
E Sunnah + Rai + Tafsiri ya wanazuoni

(viii) Ni lipi lengo kuu la kuamrishwa kusimamisha nguzo tano za Uislamu?

A Kujuana baina ya wakweli na wanafiki.
B Kuongeza thawabu na kupata Pepo ya Allah (s.w).
C Kumuabudu Allah (s.w) katika kila hatua ya maisha.
D Kuwafanya waislamu kuwa imara na wakakamavu.
E Kuimarisha uhusiano wetu na Malaika wa Allah (s.w).

(ix) Jambo gani ambalo si faradhi kufanyiwa maiti Muislamu?

A Kuoshwa
B Kukafiniwa
C Kuswaliwa
D Kuwekwa kwenye jeneza
E Kuzikwa

(x) Muandaaji anapaswa kuzingatia jambo gani katika kuandaa sanda ya mtoto?

A Jinsi ya mtoto aliyefariki
B Kuwa na vipande vitatu kama ya mwanaume
C Uzito na aina ya kitambaa
D Kuwa na vipande vitano kama ya mwanamke
E Masharti na nguzo za udhu

(xi) Zifuatazo ni adabu za kusoma Qur'an **isipokuwa**:

A Kuanza upande wa kulia
B Kuanza na kumlaani Shetani
C Kuanza na Bismillah
D Kusoma ukiwa twahara
E Kuzingatia makatazo yake

(xii) Ipi ni kazi kuu ya Sunnah katika Uislamu?

A Kuongezea Ibada.
B Kufuta dhambi.
C Kuhifadhi Hadithi.
D Kuongeza thawabu.
E Kuitafsiri Qur'an.

(xiii) Ni yapi makusudio ya kufunga mwezi mtukufu wa Ramadhani?

A Kuwezesha watu wote kuonja ladha ya njaa.
B Kuweza kufanana na umma uliopita.
C Kujifunza kuchunga mipaka ya Allah (s.w).
D Kuadhimisha kushuka kwa Qur'an.
E Kuweza kufutiwa dhambi zetu zote.

Scanned with CamScanner

(xiv) Kwa sababu gani Nabii Nuhu (a.s) alipata ushindi mkubwa katika zama zake?

A Watu wengi walimkubali na kumuamini.
B Alifanikiwa kuhamia mji mwingine na watu wake.
C Aliweza kuwaokoa watu wote kwa kutumia Jahazi.
D Aliweza kutumia maji kuwaangamiza wapinzani.
E Waumini walinusurika na makafiri waliangamia.

(xv) Ni kwanini zama kabla ya kuja Mtume (s.a.w) zilijulikana kama Jahiliyyah?

A Dunia nzima hapakuwa na mafundisho ya dini.
B Jamii zilikuwa chini katika Sayansi na Teknolojia.
C Dunia ilipoteza mwongozo sahihi kutoka kwa Muumba.
D Watu walioishi wakati huo hawakujuana.
E Hapakuwa na mfumo wowote wa kiuchumi na kiutawala.

2. Oanisha aina za mali zilizopo katika **Orodha A** na viwango vya wajibu vya utoaji wa Zakat (Nisaab) katika **Orodha B** kisha andika herufi ya jibu sahihi kwa kila kipengele katika kijitabu chako cha kujibia.

Orodha A		Orodha B	
(i)	Mazao ya shambani	A	Gram 80
(ii)	Dhahabu na Vito	B	Ishirini
(iii)	Ng'ombe	C	Thelathini
(iv)	Mali ya kuokota	D	Tola 7.5
(v)	Ngamia	E	Watano
		F	Kilo 666
		G	Thamani yoyote

SEHEMU B (Alama 35)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

3. Kwa kutumia hoja mbili na mifano, waelimishe jamii ya watu wanaopinga kuwepo kwa Mwenyezi Mungu (s.w) kwa madai kuwa haonekani.

4. (a) Jambo gani linawahamasisha Waislamu kusimamia uadilifu katika jamii?
(b) Bainisha vyanzo vitatu anavyotegemea mwanadamu katika kutambua mema na maovu kwa mtazamo wa Uislamu.

5. Tofautisha kati ya Talaka ya Zihaar na Li'aan kwa kutumia hoja moja.

6. (a) Ni ipi nafasi ya Waislamu katika kusimamia maadili katika jamii?
(b) Bainisha misingi mitatu inayoweza kuimarisha maadili katika jamii kwa mujibu wa Uislamu.

Scanned with CamScanner

7. (a) Thibitisha usahihi wa Khalifa Othman (r.a) kutumia Zakat na Sadaka ili kuimarisha jeshi la maji.
(b) Bainisha fundisho moja kwa Waislamu kutokana na kadhia iliyotajwa katika kipengele (a).

8. Taja hoja tano zinazothibitisha kuwa Qur'an ilikusanywa na kuandikwa wakati wa Mtume (s.a.w).

9. (a) Bainisha lengo la Hijjah.
(b) Eleza kwa ufupi namna ambavyo chumo la haramu linasababisha kutofikiwa lengo la Hijjah.

SEHEMU C (Alama 45)

Jibu maswali **matatu (3)** kutoka sehemu hii.

10. Eleza kazi nne za msikiti wa Mtume (s.a.w) kisha bainisha jambo moja wanalojifunza Waislamu wa zama hizi kutokana na kazi hizo.

11. Bainisha madhara manne ya kuenea kwa Hadithi Maudhuu katika jamii.

12. Eleza mambo matano ya kuzingatia katika usomaji wa Qur'an ili iwe mwongozo wa maisha ya Muislamu.

13. Fafanua faida nne zitakazopatikana katika jamii itakayosimamisha Swala za jamaa.

Scanned with CamScanner